TANGAZO LA SERIKALI NA. 321 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ya mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni zinazotolewa na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya

Tabora;

Sura ya 212

"kampuni" maana yake ni taasisi iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"matangazo ya biashara" yanajumuisha ishara, alama, maneno au kitu chochote chenye kuashiria kuijulisha jamii juu ya uwepo wa shughuli za kuuza na kununua;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua mifugo na bidhaa;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa matumizi ya soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo:

"usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu uliowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha na kutambua idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashsuri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na

Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoanishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza au kama ulivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(5) Malipo ya ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), afisa aliyeidhinishwa au wakala kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa.

Ukusanyaji wa madeni

7.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ada au ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali za mdaiwa zinazohamishika

zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3) na (4), Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kabla ya kuuza mali iliyokamatwa kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri ya Manispaa ya Tabora haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa au kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

8.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya afisa aliyeidhinishwa

9. Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria Ndogo hii, afisa aliyeidhinishwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote

linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

10. Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi, afisa aliyeishinishwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;
(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;
(f) atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii; au
(g) atatengeneza, atatayarisha au ataidhinisha utengenezaji au utunzaji wa nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

Adhabu

11. Mtu akitiwa hatiani kwa kutenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kulipa ada au ushuru unaodaiwa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Kufuta TS. Na 359 la 2015

13. Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ya 2015 imefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetegenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

1. ADA YA VIBALI VYA UJENZI

| Namba | Aina | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Majengo ya Makazi | 400 Kwa kila mita ya mraba |
| 2. | Majengo ya Biashara | 1,000 kwa kila mita ya mraba |
| 3. | Kituo cha Mafuta | 2,000,000/= |
| 5. | Taasisi, Makanisa au msikiti, shule binafsi | 1,000 kwa kila mita moja ya mraba |
| 6. | Viwanda | 1,000 kwa kila mita moja ya mraba |
| 7. | Kuongeza jengo | Asilimia 50 ya gharama za kibali cha awali |
| 8. | Kubadili jengo | Asilimia 50 ya gharama za kibali cha awali |
| 9. | Mnara (installation fee) | 2,000,000/= |
| 10. | Kupangisha Ardhi kwa matumizi ya minara ya mawasiliano | 500,000/= kwa mwezi |
| 11. | Ujenzi wa uzio wa muda | 500/= kwa kila mita moja kwa muda wa |

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | | miezi 12 |
| 12. | Ujenzi wa uzio wa kudumu (makazi) | 800/= kwa kila mita moja |
| 13. | Ujenzi wa uzio wa kudumu (biashara) | 1,000/= kwa kila mita moja |
| 14. | Maombi ya uwekaji wa bango (installation fee) | 5,000/= kwa kila futi moja ya ujazo kwa mwaka |
| 15. | Pango la kutumia eneo la barabara (Buffer zone) kwa majengo yasiyo ya kudumu | 3,000 kwa kila mita moja ya Mraba kwa kila mwezi |
| 16. | Kupangisha maeneo ya wazi (open spaces) kwa majengo yasiyo ya kudumu na yanayohamishika | Tsh.4,000/= kwa kila mita moja ya mraba kwa kila mwezi |
| 17. | Ada ya ukaguzi wa hatua za ujenzi | 20,000 kwa hatua zote za ujenzi |

2. ADA YA KUANDAA MICHORO YA MIPANGOMIJI

| Namba | Aina ya mchoro | Gharama (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kuandaa mchoro mpya (neighbourhood) | Asilimia 5 ya gharama ya kuandaa mchoro |
| 2. | Kuandaa mchoro wa urasimishaji | Asilimia 5 ya gharama ya kuandaa mchoro |
| 3. | Kurekebisha mchoro | 100,000 kwa kila kiwanja |

3. ADA NA VIBALI VYA KUBADILISHA MATUMIZI YA ARDHI.

| Namba | Matumizi | Matumizi yanayoombwa | Kiwango (shilingi) |
|---|---|---|---|

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Makazi pekee | Makazi na biashara | 150,000/= |
| 2 . | Makazi pekee | Makazi zaidi ya moja (apartment) | 200,000/= |
| 3 . | Makazi pekee | Shule,Hosteli,Zahanati na huduma nyinginezo za jamii | 250,000/= |
| 4 . | Makazi pekee | Hoteli | 200,000/= |
| 5 . | Makazi, biashara , makazi na biashara | Kituo cha mafuta | 500,000/= |
| 6 . | Makazi na biashara | (Maduka makubwa)<br>Super Market/Shooping Mall | 300,000/= |
| 7 . | Makazi pekee | Viwanda | 200,000/= |
| 8 . | Makazi pekee | Ghala (Yard/Godown) | 200,000/= |
| 9 . | Biashara | Makazi | 100,000/= |
| 10. | Ada ya uhakiki wa umiliki kiwanja au shamba (Official Search) | Matumizi yoyote | 50,000/= kwa kila kiwanja |

4. ADA YA KUFANYA UTHAMINI

| Namba | Aina ya matumizi ya kiwanja | Kiasi kwa kila kiwanja |
|---|---|---|
| 1. | Makazi Pekee | 100,000/= |
| 2. | Makazi na Biashara | 150,000/= |
| 3. | Biashara pekee | 200,000/= |

5. ADA YA KUFANYA UPIMAJI ARDHI

| Namba | Aina Ya Matumizi Ya Kiwanja | Kiasi Kwa Kila Mita Ya Mraba |
|---|---|---|
| 1. | Makazi Pekee | 400/= |
| 2. | Makazi na Biashara | 500/= |
| 3. | Biashara pekee | 600/= |
| 4. | Kuomba kuhakikiwa mipaka ya kiwanja | 50,000/= kwa kila kiwanja |

6. ADA YA UPIMAJI WA AFYA

| Namba | Ada husika | Kiwango cha Ada. |
|---|---|---|
| 1. | Fomu ya maombi ya kupima afya kwa watumishi wa hoteli, mama/baba lishe, nyumba za kulala wageni, sehemu za vinywaji bucha na maduka ya vyakula na vinywaji. | 5,000/= kila baada ya miezi sita |

7. USHURU WA MACHINJIO

| Namba | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Ushuru. | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 5,000/= | Kwa kila mnyama |
| 2. | Mbuzi, kondoo | 2,000/= | Kwa kila mnyama |
| 3. | Nguruwe | 5.000/= | Kwa kila nguruwe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Kuku/bata/bata mzinga/kanga | 500 | Kwa kila mmoja |
| 5. | Ngozi za Wanyama;<br>(a) Ng’ombe/punda<br>(b) Mbuzi/ kondo | <br>500/=<br>300/= | <br>Kwa kila ng’ombe/punda<br>Kwa kila mbuzi/kondoo |

8. ADA YA KULAZA MIFUGO INAYOZURULA

| Namba | Mfugo | Kiwango Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe, Punda | 5,000/= | Kwa kila mfugo mmoja kwa siku moja. |
| 2. | Mbuzi, kondoo | 2,500/= | Kila mbuzi au kondoo mmoja kwa siku moja |
| 3. | Nguruwe | 5,000/= | Kila nguruwe mmoja kwa siku moja |

9. ADA NA USHURU WA KURUHUSU KUINGIZA WANYAMA NA NYAMA ILIYOCHINJWA NJE YA HALMASHAURI

| Namba | Aina | Kiwango cha Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuingiza nyama yoyote | 5,000 | Kwa kila mfugo |
| 2. | Kuingiza Ng’ombe, Farasi na punda ambaye hajalipiwa kibali | 10,000/= | Kwa kila mfugo |
| 3. | Kuingiza Nguruwe | 5,000/= | Kwa kila mfugo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Mbuzi/Kondoo | 3000/= | Kwa kila mfugo. |

10. ADA YA UKAGUZI WA MAZAO MENGINE YA MIFUGO.

| Namba | Aina ya zao | Kiasi cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Maziwa ya Ng'ombe na Mbuzi | 25/= kwa kila Lita moja |
| 2. | Ngozi aina zote | 200/= kwa kila moja |
| 3. | Kwato za wanyama | 500/= kwa kila kilo moja |
| 4. | Pembe za wanyama | 500/= kwa kila kilo moja |

11. ADA YA HUDUMA NYINGINE ZINAZOHUSU MIFUGO

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kuanzisha josho la mifugo. | 50,000/= kwa kila josho kwa mwaka |
| 2. | Kuchanja wanyama | Kwa mujibu wa mongozo wa Serikali |
| 3. | Ada ya machinjio binafsi | 100,000 kwa mwaka |

12. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba | Aina ya madini | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 . | Mchanga | 1,000/= Kwa kila mita moja ya ujazo ($M^3$) |

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 2 . | Kokoto | 1,800/= Kwa kila mita moja ya ujazo ($M^3$) |
| 3 . | Mawe | 1,800/= Kwa kila mita moja ya ujazo ($M^3$) |
| 4. | Udongo | 1,000/= Kwa kila mita moja ya ujazo ($M^3$) |
| 5. | Molam/changalawe | 1,800/= Kwa kila mita moja ya ujazo ($M^3$) |
| 6. | Vumbi la kokoto | 2,000/= Kwa kila mita moja ya ujazo ($M^3$) |
| 7. | Tofali | 1,800/= Kwa kila mita moja ya ujazo ($M^3$) |
| 8. | Chokaa | 500/= Kwa kilo 25 |

13. USHURU WA KUPAKIA NA KUSHUSHA MAZAO NA BIDHAA MBALIMBALI

| Namba | Aina ya bidhaa | Gari ujazo (ukubwa wa tani) | Gharama za ushuru |
|---|---|---|---|
| 1. | Bidhaa za Ujenzi | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi. | 25,000/= |
| 2. | Bidhaa za chakula | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi. | 25,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Bidhaa za vinywaji (beverages) | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi. | 25,000/= |
| 4. | Bidhaa za matumizi ya nyumbani | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi. | 25,000/= |
| 5. | Vifaa vinavyotumia umeme | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 15 na zaidi. | 25,000/= |
| 6. | Bidhaa za Mafuta ya magari, mitambo na gesi | Tani 1 hadi tani 6.9 | 10,000/= |
| | | Tani 7 hadi tani 15 | 20,000/= |
| | | Zaidi ya Tani 15 | 30,000/= |
| 7. | Vyuma Chakavu | Tani 1-5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6-10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11-15.9 | 15,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Tani 16 na Zaidi | 25,000/= |
| 8. | Mazao Mchanganyiko ya Kilimo | Tani 1-5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6-10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11-15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 16 na Zaidi | 25,000/= |
| 9. | Mazao ya Maliasili | Tani 1-5.9 | 5,000/= |
| | | Tani 6-10.9 | 10,000/= |
| | | Tani 11-15.9 | 15,000/= |
| | | Tani 16 na Zaidi | 25,000/= |
| 10. | Bidhaa, mazao ya kilimo na maliasili na | Gunia | 1000 |
| | | Tenga | 1000 |
| | | Dumu/ndoo la lita 20 | 500 |
| | | Box | 500 |

14. USHURU WA VYOMBO VYA USAFIRI KATIKA STENDI ZA MABASI NA DALADALA.

| Namba | Aina ya Gari/huduma | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Abiria 1-18 | 2,000/=kwa kila safari |
| 2. | Abiria 1-42 | 4,000/=kwa kila safari |
| 3. | Abiria 1 -52 au zaidi. | 5,000/= kwa kila safari |
| 4. | Gari binafsi | 1000 kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Taxi | 500 kwa siku |
| 6. | Bajaji | 500 kwa siku |
| 7. | Pikipiki | 500 kwa siku |
| 8. | Ada ya matangazo | 2,000 kwa kila chombo cha usafiri kwa siku |
| 9. | Kulaza chombo cha usafiri | 5,000/= kwa siku kwa kila chombo cha usafiri |
| 10. | Kuingia stendi kwa asiye na tiketi | 300 kwa kila mtu kwa safari |

15. USHURU WA KUPAKI GARI KATIKA MAENEO YALIYOAINISHWA

| Namba. | Uwezo wa gari | Kiasi kwa siku | Kiasi kwa saa 1 |
|---|---|---|---|
| 1. | Tani 3 hadi tani 6 | 2,000/= | 1,000 |
| 2. | Tani 7 hadi tani 14 | 5,000/= | 2,000 |
| 3. | Tani 15 hadi tani 30 | 8,000/= | 4,000 |
| 4. | Zaidi ya tani 30 | 10,000/= | 5,000 |
| 5. | Gari ndogo chini ya tani 3 | 1,000/= | 500 |

16. USHURU WA VYOO VYA UMMA

| Namba | aina ya huduma | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | haja ndogo | 300/= |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | haja kubwa | 300/= |
| 3. | Kuoga (Full package) | 1,500/= |

17. ADA YA KUPANGISHA VYUMBA VYA KULALA WAGENI NA NYUMBA BINAFSI

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi kwa Siku |
|---|---|---|
| 1. | Vyumba vikubwa | Kwa bei ya soko |
| 2. | Vyumba vya kawaida | Kwa bei ya soko |
| 3. | Nyumba binafsi zilizopangishwa kwa raia wa Tanzania | 5% ya kodi ya upangishaji |
| 4. | Nyumba binafsi zilizopangishwa kwa raia wa kigeni | 10% ya kodi ya upangishaji |

18. ADA YA KUPANGISHA NA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya pango | Ada ya Pango |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kuishi | Kwa bei ya soko |
| 2. | Ukumbi wa Halmashauri (HQ) | Tsh. 700,000 kwa siku |
| 3. | Ukumbi nyingine za Halmashauri | Tsh. 200,000 kwa siku |
| 4. | Vibanda vya biashara | Kwa mujibu wa mkataba |
| 5. | Vyumba vya ofisi | Kwa mujibu wa mkataba |
| 6. | Magari ya Halmashaur | Kwa mujibu wa mkataba |
| 7. | Mitambo | Kwa mujibu wa mkataba |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Vifaa vya upimaji wa ardhi | Kwa mujibu wa mkataba |

19. ADA ZA VIBALI VYA MICHEZO, UTAMADUNI NA SANAA.

| Namba | aina ya burudani/mchezo | ada/ushuru (Shilingi) | muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Kibali cha Tamasha;<br><br>Lisilo na kiingilio | 50,000/= | Ada zote ni kwa siku. |
| | Lenye kiingilio | 150,000/= | |
| | Lenye kiingilio na matangazo | 200,000/= | |
| 2. | Usajili wa vikundi vya Sanaa | 50,000/= | Kwa usajili. |
| 3. | Kibali cha kongamano | 50,000= | Kwa siku |
| 4. | Usajili wa vibanda vya kuonesha filamu (movie), mpira au vyote kwa pamoja | 100,000/= | Kwa Mwaka |
| 5. | Kibali cha kuweka mashine / Michezo ya Kubahatisha (bonanza) | 100,000/= | Kwa kila mashine kwa miezi sita (6) |
| 6. | Kibali cha Mchezo wa pool table | 50,000/= | Kwa kila mashine/meza kwa Mwaka |
| 7. | Kibali cha tamasha la maonesho<br><br>(biashara) | 20,000/= | Kwa siku |
| 8. | Kibali cha bahati nasibu ndogo ndogo (fete) | 20,000/= | Kwa siku katika eneo moja |

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | Mshehereshaji | 10,000/= | Kwa tukio |
| 10. | Mpambaji wa ukumbi wa burudani (harusi, sherehe za jikoni, sherehe za kuaga binti na nyinginezo) | 10,000/= | Kwa tukio |
| 11. | Mtoa burudani (DJ) | 15,000/= | Kwa tukio |
| 12. | Kumbi mbalimbali za sherehe, burudani, mikutano, kongamano na matukio mbalimbali | 20,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |
| 13. | Mpishi wa vyakula kwenye matukio ya mikutano, burudani na sherehe mbalimbali | 10,000/= | Kwa tukio moja kwa siku. |
| 14. | Picha jongevu na mnato | 10,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |
| 15. | Mnada wa hadhara | 50,000/= | Kwa tukio moja kwa siku. |
| 16. | Sherehe za Harusi za ukumbini | 50,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |
| 17. | Sherehe za Harusi za nyumbani | 20,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |
| 18. | Ada ya Matangazo ya biashara na promosheni | 100,000/= | Kwa siku moja. |
| 19. | Ada ya Matangazo yasiyo ya biashara | 50,000/= | Kwa siku moja. |
| 20. | Kukodi kiwanja cha michezo | 30,000/= | Kwa siku Moja. |
| 21. | Kuuza bidhaa/ kutoa huduma kwenye matukio ya | 20,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mikutano, Burudani na sherehe mbalimbali. | | |
| 22. | Kibali cha Mganga wa jadi | 500,000/= | Kwa mwaka |
| 23. | Kuuza dawa za asili | 10,000/= | Kwa mwezi |
| 24. | Ada ya salon ya kike ya kiwango cha juu | 200,000/= | Kwa mwaka |
| | Ada ya salon ya kike ya kiwango cha kati | 100,000/= | Kwa mwaka |
| | Ada ya salon ya kike ya kiango cha chini | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 25. | Ada ya salon ya kiume ya kiwango cha juu | 100,000/= | Kwa mwaka |
| | Ada ya salon ya kiume ya kiwango cha kati | 50,000/= | Kwa mwaka |
| | Ada ya salon ya kiume ya kiango cha chini | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 26. | Kibali cha ngoma za asili | 10,000/= | Kwa tukio |
| 27. | Kibali cha kupiga muziki (disco) la kiingilio | 30,000/= | Kwa tukio |
| 28. | Kibali cha matangazo ya biashara kwa kutumia kipaza sauti | 5,000/= | Kwa mwezi |
| 29. | Kuingiza/kurusha miziki | 10,000/= | Kwa mwezi |

20. ADA YA HUDUMA ZA MZANI

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| Namba | Huduma | kiasi cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kupima uzito wa gari zaidi ya tani 21 | 15,000/= |
| 2. | Gari lenye uzito wa kati ya tan 11 -20 | 10,000/= |
| 3. | Gari lenye uzito kati ya tan 0 hadi tan 10 | 7,000/= |

21. USHURU WA KITUO CHA KUOSHA VYOMBO VYA USAFIRI

| Namba | Eneo kilipo kituo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya kibali cha kuanzisha kituo cha kuoshea magari (car wash) | 100,000/= kwa maeneo ya Kata za Mpera, Ipuli, Cheyo, Kitete, Mbugani, Ng'ambo, Kidongo Chekundu, Mwinyi, Kanyeye, Chemchem, Mapambano, Kiloleni, Gongoni, Isevya, Mtendeni na Tambukaleli |
| | | 50,000/= kwa maeneo ya Kata zinazobakia |

22. USHURU WA VIWANDA VYA TOFALI

| Namba | Aina ya tozo | Kiwango cha tozo |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya kibali cha kuanzisha kiwanda cha kutengeneza tofali na tofali za mapambo kwa ajili ya biashara | 100,000/= kwa mkupuo |

23. USHURU WA KITUO CHA KUTENGENEZA SAMANI

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| Namba | Aina ya Tozo | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya kibali cha kuanzisha karakana ya kutengeneza samani | 50,000/= kwa mwaka |
| 2. | Ushuru wa samani | 5% ya bei ya soko |

24. USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

| Namba | Aina ya zao | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | Mkaa | 2,000/= kwa gunia |
| 2. | Kuni | 1,000/= kwa mita moja ya ujazo ($M^3$) |
| 3. | Mbao | 5% ya bei ya kununulia kwa kila ubao |
| 4. | Asali | 2,000/= kwa chombo chenye ujanzo wa lita 20 |
| 5. | Nta | 500/= kwa kilo |
| 6. | Mabanzi | 300/= kwa banzi |
| 7. | Nguzo (aina zote) | 500/= kwa nguzo |
| 8. | Gogo | 2,000/= kwa kila gogo |
| 9. | Fito | 1,000/= kwa mzigo mmoja |
| 11. | Chenga za Mkaa | 1,000/= kwa gunia |

25. USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

| Namba | aina ya mazao | ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya chakula | Asilimia 3% ya bei ya kununulia kwa ujazo unaozidi tani moja |
| 2<br>2. | Mazao ya biashara | Asilimia 3% ya bei ya kununulia kwa ujazo unaozidi tani moja |
| 3. | Ushuru wa mashudu, pumba na mabaki ya mazao | 1,000/= kwa gunia |
| 4. | Ushuru wa matunda mchanganyiko | 1,000/= kwa tenga moja |

26. USHURU WA GEREJI

| Namba | Aina ya Tozo | Kiwango cha tozo |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya kibali cha kuanzisha gereji ya magari | 50,000/= kwa mkupuo kwa eneo moja |
| 2. | Ada ya kuanzisha gereji ya pikipiki | 25,000 kwa mkupuo kwa eneo moja |
| 3. | Ushuru wa gereji za pikipiki | 10,000/= kwa mwezi |

27. USHURU WA CHUMA CHAKAVU

| Namba | Aina ya Tozo | Kiwango cha tozo |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya kibali cha kuanzisha/ kuhuisha kituo cha kununulia chuma chakavu | 50,000/= kwa mkupuo kwa eneo moja kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Gari lenye ukubwa wa tani 3 hadi 5 | 30,000/= kwa gari kwa tripu |
| 3. | Gari lenye ukubwa wa zaidi ya tani 5 | 50,000/= kwa gari kwa tripu |

28. ADA YA USAJILI WA KIKUNDI CHA KIJAMII (CBO)

| Namba | Aina ya tozo | Kiwango cha tozo |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya usajili | 20,000/= kiwa mkupuo mmoja |
| 2. | Ada ya kikundi | 20,000/= kwa mwaka |

29. USHURU WA SAMAKI, DAGAA NA MAZAO MENGINE YA MAJINI

| Namba | Aina ya zao | Kiasi kwa tenga/ndoo moja (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Samaki wabichi | 1000 |
| 2. | Samaki wakavu | 1000 |
| 3. | Dagaa wakavu/gunia | 1000 |
| 4. | Furu | 1000 |
| 5. | Dagaa wabichi | 1000 |
| 6. | Uduvi | 1000 |
| 7. | Konokono | 1000 |
| 8. | Mazao mengine ya ziwani au bwawa au mito au malambo | 20 |

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

30. ADA YA KUSAJILI VYOMBO VYA MOTO VINAVYOTOA HUDUMA

| Namba. | Ujazo wa chombo | Kiasi cha tozo |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki za magurudumu mawili | 5,000/= kwa mwaka |
| 2. | Pikipiki za magurudumu matatu za abiria | 10,000/= kwa mwaka |
| 3. | Pikipiki za magurudumu matatu za mizigo | 10,000/= kwa mwaka |
| 4. | Taxi za kubeba abiria | 15,000/= kwa mwaka |
| 5. | Magari ya mizigo chini ya tani 3 | 20,000/= kwa mwaka |
| 6. | Magari ya mizigo zaidi ya tani 3 | 30,000/= kwa mwaka |
| 7. | Ada ya usajili wa egesho la pikipiki za magurudumu mawili | 50,000/= kwa kila egesho kwa mwaka |
| 8. | Ada ya usajili wa egesho la pikipiki za magurudumu matatu | 100,000/= kwa kila egesho kwa mwaka |

31. USHURU WA KUINGIZA BIDHAA SOKONI

| Namba | Aina ya bidhaa | Ushuru kwa Siku (Shilingi). | Kipimo |
|---|---|---|---|
| 1. | Nafaka | 1,000.00 | Kwa gunia |
| 2. | Vitunguu | 1,000.00 | Kwa gunia |
| 3. | Nyanya | 1,000.00 | Kwa tenga |
| 4. | Dagaa | 1,500.00 | Kwa gunia |
| 5. | Viazi mviringo | 1,000.00 | Kwa gunia |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | viazi vitamu | 1,000.00 | Kwa gunia |
| 7. | Matunda | 1000.00 | Kwa tenga au gunia |
| 8. | Samaki | 3,000.00 | Kwa tenga |
| 9. | Wauza ndizi | 1,000.00 | Kwa mkungu |
| 10. | Mihogo | 1,000.00 | Kwa gunia |
| 11. | Wauza alizeti | 1,000.00 | Kwa gunia |
| 12. | Wauza miwa | 5,000.00 | Kwa lori tani |
| 13. | Viuongo vya mboga | 1,000.00 | Kwa tenga |
| 14. | Wauza pumba za nafaka | 500.00 | Kwa gunia |
| 15. | Wauza kabichi | 5,000.00 | Kwa tani |
| 16. | Bidhaa nyinginezo | 1,000.00 | kwa gunia |

32. USHURU WA SOKO

| Namba | Aina ya tozo | Kiasi cha tozo |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kupangisha kizimba | 15,000 kwa mwezi |
| 2. | Kizimba cha kuku | 20,000/= kwa mwezi |
| 3. | Ushuru wa mama/baba lishe | 10,000 kwa mwezi |

33. ADA YA MAOMBI YA ZABUNI MBALIMBALI ZA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya chanzo | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|

*Tangazo La Serikali Na. 321 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ukusanyaji wa mapato | 100,000/= |
| 2. | Ujenzi wa barabara | 100,000/= |
| 3. | Ukusanyaji na uondoshaji wa taka ngumu | 100,000/= |
| 4. | Kukarabati na kujenga maduka Vioski na vizimba vya umma | 100,000/= |
| 5. | Kurekebisha mali za Halmashauri (magari na majengo) | 100,000/= |
| 6. | Ukaguzi na upimaji wa viwanja. | 100,000/= |
| 7. | Uendeshaji vyoo vya umma | 100,000/= |
| 8. | Uendeshaji wa vioski vya Halmashauri | 100,000/= |
| 9. | Huduma elekezi / mshauri (Consultancy services) | 100,000/= |
| 10. | Upangishaji Maduka / Vizimba | 50,000/= |
| 11. | Ujenzi wa majengo | 100,000/= |
| 12. | Huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalamu (non-consultancy services) | 100,000/= |
| 13. | Maeneo mengine ambayo hayajatajwa | 100,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetegenezwa chini ya kanuni ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........…………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, kwamba mnamo tarehe ………… ya mwezi…………. Mwaka ……… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ……………cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………

Jina: ……………………………...
Saini: …………………………….
MBELE YANGU:
Jina: ……………………………………
Wadhifa: ……………………………….
Saini: …………………………………..
Tarehe: ………………………………...

Lakari ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufutia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora uliofanyika tarehe 12 mwezi 05 Mwaka 2023 na kushuhudiwa lakari hiyo ikigongwa mbele ya;-

ELIAS MAHWAGO KAYANDABILA
*Mkurugenzi wa Manispaa*
*Halmashauri ya Manispaa ya Tabora*

MHE. RAMADHANI S. KAPELA
*Mstahiki Meya*

*Halmashauri ya Manispaa Tabora*

NAKUBALI

L.S

Dodoma,
20 Februari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*